

La déclaration sur la famille : des paroles venant de Dieu

Par Ronald A. Rasband
du Collège des douze apôtres

Tangazo la Familia—Maneno kutoka kwa Mungu

Na Mzee Ronald A. Rasband
Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili

Conférence générale d'octobre 2025

La déclaration est d'origine divine. Nous devons donc la traiter avec le respect que méritent les paroles de Dieu.

Cette conférence générale d'octobre 2025 marque le trentième anniversaire de la publication de « La famille, déclaration au monde ». Par dessein divin, cette déclaration, reçue par révélation, a été rédigée pour « sauvegarder et [...] fortifier la famille dans son rôle de cellule de base de la société ».

Nous faisons tous partie d'une famille, que nous soyons mère, père, fille, fils, petit-enfant, grand-parent, tante, oncle, frère, sœur ou cousin. Plus important encore, selon la déclaration, chacun de nous est « un fils ou une fille d'esprit aimé de parents célestes [qui possède] une nature et une destinée divines ».

Quand j'ai été appelé au saint apostolat en 2015, on m'a dit ceci : « Désormais, cette déclaration t'appartient. » Puis, en désignant les mots « Conseil des douze apôtres » dans le titre, la personne a ajouté : « Ton nom est là. Imprègne-t'en et enseigne-la comme si c'était la tienne. »

Que j'aime la déclaration sur la famille ! De l'Afrique à l'Australie, j'ai témoigné à travers le monde du rôle de la famille dans le plan éternel de Dieu. La déclaration est d'origine divine. Nous devons donc la traiter avec le respect que méritent les paroles de Dieu.

Frères et sœurs, comme je l'ai dit à cette chaire lors d'une conférence générale passée, souvenez-vous que « les mots sont importants ».

La déclaration est au cœur de nos croyances. Je vais vous raconter dans quelles circonstances

Tangazo hili lina asili ya kiungu, hivyo lazima tulichukulie kwa unyenyekevu unaostahili maneno yanayotoka kwa Mungu.

Mkutano mkuu huu wa Oktoba 2025 unafanya kumbukizi ya miaka 30 ya tangazo la « Familia: Tangazo kwa Ulimwengu. » Kwa usanifu wa kiungu, tangazo hili, pamoja na maneno yake ya kiufunuo, lilitolewa ili « kudumisha na kuimarisha familia kama kitengo muhimu cha jamii. »

Kila mtu ni sehemu ya familia, iwe wewe ni mama, baba, binti, mwana, mjukuu, babu au bibi, shangazi, mjomba, kaka, dada au binamu. La muhimu zaidi, kila mmoja wetu ni, kama tangazo linavyoeleza, « mwana au binti mpendwa wa kiroho wa wazazi wa mbinguni ... [mwenye] asili na hatima ya kiungu. »

Wakati nilipoitwa kwenye utume huu mtakatifu mwaka 2015 nilishauriwa, « Tangazo hili sasa ni la kwako. Jina lako [akinyoshea kwa kidole kwenye maneno 'Baraza la Mitume Kumi na Wawili' katika kichwa cha habari] liko hapa. Lihisi na lifundishe kama wewe unalimiliki. »

Ninalipenda tangazo la familia. Nimeli-shuhudia kote ulimwenguni kutoka Afrika hadi Australia na kila mahali baina ya jukumu la familia katika mpango wa milele wa Mungu. Tangazo hili lina asili ya kiungu, hivyo lazima tulichukulie kwa unyenyekevu unaostahili maneno yanayotoka kwa Mungu.

Kumbukeni, akina kaka na akina dada, kama nilivyosema katika mkutano mkuu mmoja uliopita kutoka kwenye mimbari hii, « Maneno ni muhimu. »

Acha nikupeni baadhi ya chimbuko kuhusu tangazo hili kama ujumbe mkuu wa kile tuna-

elle a été écrite.

En 1994, un an avant la présentation de la déclaration, le Collège des douze apôtres a discuté de l'éloignement croissant de la société et des gouvernements des lois de Dieu concernant la famille, le mariage et l'identité sexuelle. Le président Nelson a expliqué plus tard : « Ce n'est pas là tout ce que nous avons vu se profiler. Nous avons vu les efforts entrepris par diverses communautés pour éliminer toutes les normes et les limites relatives à l'activité sexuelle. Nous avons vu la confusion des sexes. Nous avons vu tout cela arriver. »

Les Douze ont décidé de rédiger un document, une déclaration officielle, qui résumait la position de l'Église sur la famille. Cette année-là, ces apôtres, des voyants appelés de Dieu, ont préparé une déclaration sur la famille. Dallin H. Oaks a raconté qu'à l'aide de la prière, ils se sont tournés vers le Seigneur pour savoir « ce qui devait être dit et [...] la manière de le dire ». Ils ont présenté la déclaration à la Première Présidence, constituée de Howard W. Hunter, Gordon B. Hinckley et Thomas S. Monson, pour qu'elle l'examine.

Quelques mois plus tard, en mars 1995, le président Hunter est décédé et le président Hinckley est devenu le quinzième président de l'Église. La déclaration était alors entre ses mains. Quel serait le bon moment pour faire cette déclaration à l'Église? Ce moment est arrivé six mois plus tard.

Quelques jours avant la réunion générale des femmes du 23 septembre, qui précédait la conférence générale, le président Hinckley et ses conseillers ont tenu conseil avec la présidence générale de la Société de Secours. Les sœurs, comme les apôtres, avaient réfléchi aux préoccupations qui touchaient les femmes et la famille. Il a été décidé d'axer la réunion à venir sur la famille.

Il était prévu que le président Hinckley s'adresse aux femmes lors de la réunion. Il avait médité sur le sujet de son discours. Au cours de la discussion, il a mentionné le titre de la déclaration au monde sur la famille, nouvellement rédigée et qui n'avait pas encore été rendue publique. Cette réunion des femmes était-elle le bon cadre pour faire une déclaration décisive sur la famille?

Elaine Jack, alors présidente générale de la Société de Secours, a expliqué plus tard : « À ce

choamini.

Mwaka 1994, mwaka mmoja kabla ya kuwasilishwa kwa tangazo, Akidi ya Mitume Kumi na Wawili walijadili jinsi ambavyo jamii na serikali zilivyokuwa zikijiondoa kutoka kwenye sheria za Mungu kwa ajili ya familia, ndoa na jinsia. “Lakini haya hayakuwa mwisho wa yale tuliyoyana,” Rais Nelson baadaye alielezea. “Tuliweza kuona juhudi za jamii tofauti kuondoa viwango vyote na viziwi kwenye shughuli ya kujamiiana. Tuliweza mkanganyiko wa jinsia. Tuliweza kuona yote yakija.”

Wale Kumi na Wawili waliazimia kutayarisha waraka, tangazo rasmi, likitoa muhtasari wa msimamo wa Kanisa juu ya familia. Katika mwaka huo, Mitume hawa, waonaji walioitwa na Mungu, walitayarisha tamko kuhusu familia. Rais Dallin H. Oaks alikumbuka kwamba kwa sala walimgeukia Bwana kwa ajili ya “kile [wao] walichopaswa kusema na jinsi [wao] walivyopaswa kusema.” Waliuwasilisha kwa Urais wa Kwanza—Marais Howard W. Hunter, Gordon B. Hinckley na Thomas S. Monson kwa ajili ya mawazo yao.

Miezi michache tu baadaye mnamo Machi 1995, Rais Hunter alifariki na Rais Hinckley akawa Rais wa 15 wa Kanisa. Tangazo hilo likawa sasa katika mikono yake. Lini ingekuwa wakati sahihi kufanya tamko hili kwa Kanisa? Muda huo ulifika miezi sita baadaye.

Siku kadhaa kabla ya mkutano mkuu wa Muungano wa Usaidizi wa Septemba 23 ambao ulitangulia mkutano mkuu, Rais Hinckley na washauri wake walikutana katika kushauriana na Urais Mkuu wa Muungano wa Usaidizi. Aki-na dada hawa, kama wale Mitume, wamekuwa wakizidiwa na uzito wa mashaka kuhusu wana-wake na familia. Walikuwa wamefokasi kwenye mkutano unaokuja juu ya familia.

Rais Hinckley alikuwa amepangiwa kuhutubia wanawake hawa kwenye mkusanyiko huo. Yeye amekuwa akitafakari mwelekeo wa mahubiri yake. Mjadala huu ulivyoendelea, alitaja kwa jina tangazo hili lililoandaliwa hivi karibuni lakini bado halijatangazwa kwa umma “Familia: Tangazo kwa Ulimwengu.” Je, mkutano huu wa wanawake ulikuwa mazingira sahihi ya kufanya tamko la kimaamuzi kuhusu familia?

Rais Mkuu wa Muungano wa Usaidizi Elaine Jack baadaye alielezea: “Sisi hatukujua Tangazo

moment-là, nous ne savions pas ce qu'était la déclaration sur la famille. Nous pouvions le deviner par son titre et nous sentions que tout message sur la famille [...] serait bénéfique. [...] J'étais convaincue que les membres du Collège des Douze recevaient des révélations. »

Ce samedi-là, la réunion de la Société de Secours a été historique. Avant de présenter la déclaration, le président Hinckley a prononcé ces paroles importantes : « Avec tous les raisonnements spécieux qui sont présentés comme des vérités, avec toutes les tromperies à propos des principes, avec toutes les incitations à nous laisser gagner peu à peu par la souillure du monde, nous nous sentons poussés à lancer un avertissement [et à réaffirmer] les principes, la doctrine et les pratiques relatifs à la famille que les prophètes, voyants et révélateurs de notre Église ont énoncés à maintes reprises tout au long de son histoire. »

Il a ensuite lu la déclaration dans son intégralité. Comme le Seigneur l'a déclaré : « Que ce soit par ma voix ou par la voix de mes serviteurs, c'est la même chose. »

La déclaration énonce : « La famille est ordonnée de Dieu. » Que j'aime la clarté de cette phrase ! Cette déclaration est un appel à traverser la condition mortelle en gardant toujours à l'esprit la divinité qui est en nous et l'avenir éternel qui nous attend. Le président Nelson a enseigné : « Vous êtes littéralement des enfants d'esprit de Dieu. [...] Ne vous y trompez pas : votre potentiel est divin. Si vous cherchez diligemment, Dieu vous donnera un aperçu de ce que vous pouvez devenir. »

Lorsqu'elle a été présentée, la déclaration n'était pas en accord avec l'opinion de beaucoup dans le monde. C'était le cas à l'époque. C'est toujours le cas aujourd'hui. Certains s'opposent à ce qu'elle affirme sur la famille, le mariage et le genre. D'autres suggèrent que l'Église devrait retirer, réviser ou même mettre de côté la déclaration.

Chers frères et sœurs, comme l'a dit le président Hinckley, cette déclaration sur la famille est doctrinale. Les principes qu'elle énonce ne sont pas en contradiction avec les voies du Seigneur et son chemin des alliances, mais en parfaite harmonie avec eux. Les enseignements que contient la déclaration ont été révélés par notre Seigneur Jésus-Christ à ses apôtres, à l'époque et aujourd'hui. C'est son Église. C'est lui qui a établi les vérités selon lesquelles nous vivons.

lile juu ya familia lilikuwa kitu gani kwa wakati ule. ... [Sisi] tuliweza kulijua tu kwa kichwa cha habari, lakini tulihisi chochote juu ya familia ... kingekuwa kitu chanya. ... Nilijihisi chanya sana kwamba tulikuwa na washiriki wa Akidi ya Kumi na Wawili ambao walikuwa wakipokea ufunuo."

Mkutano wa Muungano wa Usaidizi Juma-mosi ile ulikuwa wa kihistoria. Rais Hinckley alitambulisha tangazo la familia kwa maneno haya muhimu: "Kwa maneno mengi ya ulaghai yanayochukuliwa kama ukweli, pamoja na udanganyifu mwingi kuhusiana na viwango na maadili, pamoja na vivutio vingi na vishawishi vya kuchukua pole pole uchafu wa ulimwengu, tumehisi kuonya na kuonya mapema ... juu ya viwango, mafundisho na desturi zinazohusiana na familia ambazo manabii, waonaji, na wafunuzi wa Kanisa hili kwa kurudia rudia wameelezea kote katika historia yake."

Kisha yeye akasoma lile tangazo kwa ukamilifu wake. Kama vile Bwana alivyosema, "Iwe ni kwa sauti yangu mwenyewe au kwa sauti ya watumishi wangu, yote ni sawa."

Tangazo linaeleza, "Familia imeamriwa na Mungu." Ninapenda uwazi wa maelezo hayo. Tangazo ni wito kwetu sisi kuishi duniani daima tukikumbuka uungu ulio ndani yetu na umilele ujao ulioko mbele yetu. Rais Nelson alifunza, "Wewe kiuhalisia ni mtoto wa Mungu. ... Usifanye makosa kuhusu hili: Uwezekano wako ni wa kiungu. Kwa utafutaji wako kwa bidii, Mungu atakupatia taswira kidogo kidogo ya kile unachoweza kuwa."

Lilipowasilishwa, tangazo hili halikufungamana na mitazamo ya wengi ulimwenguni. Siyo wakati huo. Siyo kwa sasa. Kuna wale ambao wanaona kasoro katika hili tangazo juu ya familia, ndoa na jinsia. Baadhi wanapendekeza Kanisa liliondoe, lifanye marejeo au hata kuliweka kando tangazo hili.

Tangazo hili juu ya familia ni, kama Rais Hinckley alivyoeleza, ni mafundisho, wapendwa kaka zangu na dada zangu. Kanuni hizi haziko nje ya hatua bali kikamilifu ndani ya hatua pamoja na njia za Bwana na njia Yake ya agano. Mafundisho ya tangazo hili yalifunuliwa na Bwana wetu Yesu Kristo kwa Mitume Wake wakati huo na sasa. Hili ni Kanisa Lake, Yeye ndiye aliyeweka ukweli ambao kwa ukweli huu sisi tunaishi.

En réfléchissant à la déclaration, certains d'entre vous se disent peut-être : « Elle ne convient pas à ma situation. » « Elle manque d'empathie. » « Ma famille ne ressemble pas à cela. » « Je ne m'y reconnais pas. »

Aux personnes inquiètes à ce sujet, je dis : sachez que vous êtes un enfant de parents célestes que vous faites partie de la famille de votre Père céleste. Personne ne vous connaît mieux que lui ni ne se soucie plus profondément de vous. Tournez-vous vers lui, déversez-lui votre cœur, ayez confiance en lui et en ses promesses. Vous avez une famille en la personne de votre Sauveur, Jésus-Christ, qui vous aime. Il est venu sur terre pour expier nos péchés et porter le fardeau de nos fautes et de nos jours les plus sombres. Il comprend ce que vous traversez et ressentez. Tournez-vous vers lui et ayez confiance qu'il enverra le Saint-Esprit pour vous accompagner, vous élever et vous guider. Ressentez leur amour « qui se répand dans le cœur des enfants des hommes [...] ; c'est la plus désirable de toutes les choses [...] et la plus joyeuse pour l'âme ».

Tous les apôtres du seigneur vous aiment tendrement. Nous prions pour vous et recherchons les directives du Seigneur à votre égard. Restez avec nous. Vous vivez à une époque difficile où l'adversaire cherche à vous assujettir. Ne vous laissez pas entraîner. Et si vous l'avez été, revenez. Nos bras, ainsi que ceux d'autres personnes qui vous aiment, vous sont ouverts.

La déclaration stipule que « les parents ont le devoir sacré d'élever leurs enfants dans l'amour et la droiture ». Le Livre de Mormon offre un deuxième témoignage de cette vérité. Au premier verset de son premier chapitre, nous lisons : « Moi, Néphi, étant né de bons parents. » Combien d'entre nous ont commencé, et recommencé encore et encore, le Livre de Mormon, au point que ces mots sont devenus gravés dans notre esprit ? Gravez-les dans votre cœur.

L'une de mes phrases préférées de la déclaration est celle-ci : « On a le plus de chances d'atteindre le bonheur en famille lorsque celle-ci est fondée sur les enseignements de [...] Jésus-Christ. »

Qui ne souhaite pas être heureux ?

Et quels sont les enseignements de Jésus-Christ ? De nouveau, dans la déclaration : « La foi, la prière, le repentir, le pardon, le respect, l'amour, la compassion, le travail et les divertissements sains. »

Baadhi yenu mnaweza kuangalia tangazo na kusema, “Hii haifanyi kazi kwangu.” “Inaonekana haina maana.” “Familia yangu haionekani hivyo.” “Hainihusu.”

Kwa wale wenye mashaka, jueni kwamba wewe ni mtoto wa wazazi wa mbinguni, ni sehemu ya familia ya Baba wa Mbinguni. Hakuna mtu anayekujua vizuri zaidi au anayejali kwa kina zaidi kuhusu wewe kuliko Yeye anavyokujali. Mgeukie Yeye, mimina moyo wako Kwake, mtumainie Yeye na ahadi Zake. Unayo familia katika Mwokozi wako Yesu Kristo, ambaye anakupenda. Yeye alikuja duniani kulipia dhambi zetu na kubeba mzigo wa makosa yetu na zile siku mbaya sana. Yeye anaelewa kile unachokabiliana nacho na unavyohisi. Mgeukie Yeye, mtumainie Yeye atamtuma Roho Mtakatifu kuwa pamoja nawe, kukuinua na kukuongoza. Hisi upendo Wao ambao “umejimimina wenyewe katika mioyo ya watoto wa watu; ... ni wa kupendeza zaidi ya vitu vyote ... na inafurahisha zaidi kwa shangwe.”

Mitume wote wa Bwana wanakupenda sana. Tunasali kwa ajili yenu na tunaomba mwongozo wa Bwana kwa ajili yenu. Kaeni pamoja nasi. Mnaishi katika nyakati zenye changamoto ambapo yule adui anatafuta kuwafanya ninyi muwe wake. Msichotwe. Na kama umechotwa, rudi. Mikono yetu imenyoshwa kwako kama inavyofanya ile ya wengine wanao kupenda.

Tangazo linasema, “Wazazi wana jukumu takatifu la kuwalea watoto wao kwa upendo na kwa uadilifu.” Kitabu cha Mormoni kinatoa ushahidi wa pili kwenye ukweli huu. Katika aya ya kwanza ya mlango wa kwanza, tunasoma, “Mimi, Nefi, nikiwa nimezaliwa na wazazi wema.” Je, ni wangapi kati yetu tumeanza Kitabu cha Mormoni—na kuanza tena na tena—na katika mchakato huo tunaweka maneno yale katika kumbukumbu? Kuyatia moyoni.

Moja ya kauli yangu pendwa katika tangazo ni hii “Furaha katika maisha ya familia itapatikana kwa urahisi ikiwa imejegwa katika mafundisho ya ... Yesu Kristo.”

Je, ni nani hapendi kuwa na furaha?

Na mafundisho ya Yesu Kristo ni nini? Tena, katika tangazo hili: “Imani, sala, toba, msamaha, heshima, upendo, huruma, kazi na shughuli nzuri za burudani.”

Qui ne verrait pas sa vie s'améliorer en mettant en pratique ces principes essentiels ? Aucun d'entre nous ne les mettra parfaitement en application, mais nous pouvons toutefois suivre ces sages paroles du président Hinckley : « Faites de votre mieux. »

Dans la déclaration, nous lisons : « Le père doit présider dans l'amour et la droiture » et « la mère a pour première responsabilité d'élever ses enfants ». Présider ne veut pas dire dominer et élever ne désigne pas un rôle secondaire. Dieu a donné aux hommes et aux femmes des rôles différents, mais égaux, essentiels et complémentaires.

Je vais vous raconter une histoire personnelle.

Ma femme et moi avons appris à mieux travailler en partenaires égaux après qu'un jour j'ai décidé de prendre une décision importante sans la consulter. Cela l'a surprise, l'a prise au dépourvu et l'a placée dans une situation très difficile. Quelque temps après, elle a posé la main sur mon épaule et m'a dit avec fermeté : « Ron, s'il te plaît, ne me fais plus jamais ça. » Depuis ce jour, nous avons pratiquement toujours été en accord.

Nous trouvons ceci dans la déclaration sur la famille : « Le père et la mère ont l'obligation de s'aider en qualité de partenaires égaux. »

«Égaux» est un mot important. Au fil des années, sœur Rasband et moi avons travaillé ensemble sur ce que la déclaration décrit comme nos « responsabilités sacrées », nous avons façonné notre mariage sous un joug d'égalité. Maintenant que nos enfants sont tous mariés, sœur Rasband et moi-même continuons de leur donner des conseils, ainsi qu'à leurs conjoints, sur la manière d'être des partenaires égaux.

Lorsque nous vivons les yeux fixés uniquement sur la gloire de Dieu, nous nous respectons les uns les autres et nous nous soutenons mutuellement. Ces modèles divins de justice conduisent à la stabilité dans notre vie, dans notre famille et dans la société.

Notre Père céleste a donné la déclaration sur la famille afin de nous aider à revenir à lui, à apprendre, et à être remplis d'amour, de force, de détermination et de compréhension éternelle. De toute mon âme, je vous supplie de rester proches de lui et de son Fils bien-aimé. Je vous promets que si vous le faites, l'Esprit vous inspirera, vous guidera et vous aidera à ressentir dans votre

Je, ni maisha ya nani hayatakuwa bora zaidi kwa kutumia kanuni hizi muhimu? Hakuna ye yote kati yetu atakaye fanya kikamilifu; lakini tunaweza kufuata maneno ya hekima ya Rais Hinckley, "Fanya vizuri uwezavyo."

Tunasoma katika tangazo, "Akina baba wataongoza ... kwa upendo na haki," na "akina mama kimsingi wanawajibika kuwalea watoto wao." - Kuongozihakumaanisha kukandamiza nakulea-hakumaanishi nafasi ya upili. Mungu amewapatia wanaume na wanawake nafasi tofauti lakini zilizo sawa ambazo zinakamilishana.

Acha nishiriki hadithi binafsi.

Mimi na mke wangu tulijifunza kufanya vyema zaidi katika kuwa wenza walio sawa baada ya siku moja mimi kuamua kufanya uamuzi muhimu pasipo kushauriana naye. Kitendo changu kilimshangaza, kilimshitukiza, na kumweka katika hali ngumu sana. Baadaye, aliweka mikono yake mabegani mwangu na kwa uthabiti alisema, "Ron, tafadhali, kamwe usinifanyie hivyo tena." Tangu hapo tumekuwa vizuri sana kwenye ukurasa mmoja.

Tunapata katika tangazo la familia, "Akina baba na akina mama wanao wajibu wa kusaidiana kama wenza walio sawa."

Sawani neno muhimu. Kwa miaka mingi, mimi na Dada Rasband tumefanya kazi pamoja katika kile tangazo linaelezea kama "majukumu yetu matakatifu," tumetengeneza ndoa iliyofungwa nira sawa. Kwa kuwa kila mmoja wa watoto wetu ameoa au kuolewa, Dada Rasband na mimi tumeendelea kuwashauri wao na wenza wao jinsi ya kuwa wenza walio sawa.

Tunapoishi angali macho yetu yakiwa kwenye utukufu wa Mungu, tunaheshimiana na kusaidiana. Mipangilio hii ya kiungu ya haki hutuongoza kwenye uimara wa maisha yetu binafsi, familia zetu na katika jamii.

Baba yetu wa mbinguni ametoa tangazo hili juu ya familia ili kusaidia kutuongoza sisi nyumbani Kwake ili kutusaidia kujifunza na kujawa na upendo, nguvu, dhumuni na uelewa wa milele. Kwa nafsi yangu yote, ninakusihi kuishi karibu na Yeye na Mwanawe Mpendwa. Ninakuahidi unapofanya hivi, Roho atakushawishi na kuongoza na kukusaidia kuhisi moyoni mwako

cœur la paix promise qui « surpasse toute intelligence ». Au nom de Jésus-Christ. Amen.

amani yao iliyoahidiwa ambayo “inapita uelewa wote.” Katika jina la Yesu Kristo, amina.